

KUMB: PPR/15 - 02/1

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA
JUMATANO, TAREHE 4 FEBRUARI 2015

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 4 Februari 2015**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na za rejareja kwa aina zote za mafuta, yaani, Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeshuka ikilinganishwa na bei katika toleo lililopita la tarehe 07 Januari 2015. Katika toleo hili, bei za rejareja kwa Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimepungua kwa viwango vifuatavyo: Petroli Sh 187/lita sawa na asilimia 9.56 Dizeli Sh 139/lita sawa na asilimia 7.53 na Mafuta ya Taa Sh 177/lita sawa na asilimia 9.64. Aidha, kwa kulinganisha matoleo haya mawili, bei za jumla zimepungua kama ifuatavyo: Petroli, Sh 186.89/lita sawa na asilimia 10.08, Dizeli, Sh 138.97/lita sawa na asilimia 7.97, na Mafuta ya Taa, Sh 176.64/lita sawa na asilimia 10.20. Mabadiliko haya ya bei yametokana na kushuka kwa bei za mafuta katika soko la Dunia.

Bei za mafuta masafi (refined petroleum products) katika soko la dunia, kwa Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimepungua kati ya mwezi Julai na Desemba 2014 kwa takribani ya Dola 440/tani, Dola 304/tani na Dola 324/tani sawia sawa na punguzo la asilimia 44, 35 na 35 sawia. Kati ya mwezi Septemba 2014 na Februari 2015 bei za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa katika soko la ndani zimepungua kwa jumla ya kiasi cha Sh 499/lita, Sh 384/lita na Sh 384/lita sawia ambayo ni sawa na punguzo la asilimia 22, 18 na 19 sawia. Katika kipindi husika, thamani ya shillingi ya Tanzania kulinganisha na Dola ya Marekani imeshuka kwa asilimia 6. Bei ya mafuta kwenye soko la ndani ingeweza kupungua zaidi kama thamani ya shillingi isingeendelea kudhoofu. Pia ni muhimu kuzingatia kuwa, kwa wastani, bei za mafuta katika soko la dunia na gharama za uagizaji (CIF) huchangia asilimia 60 ya bei ya mafuta katika soko la ndani, hivyo kiwango cha ushukaji bei katika soko la ndani hakiwezi kuwa sambamba na asilimia ya ushukaji katika soko la dunia.

- (b) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2008, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (c) **Kampuni za mafuta zipo huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani ilimradi bei hizo ziko chini ya bei kikomo (price cap)** kama ilivyokotolewa na formula iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapwa kwenye **Gazeti la Serikali Na. 354 la tarehe 26 Septemba 2014**.

- (d) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionyesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta kutoka kwenye vituo vinavyouza mafuta kwa bei ndogo zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja na adhabu itatolewa kwa kituo husika.**
- (e) Wanunuzi wanashauriwa kuhakikisha kuwa wanapata stakabadhi ya malipo inayoonesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hiyo ya malipo itatumika kama kidhibiti cha mnunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya ama kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo; ama endapo utakuwa umeuziwa mafuta yenyе kiwango cha ubora kisichofaa.

A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Sh/Lita)	Dizeli (Sh/lita)	Mafuta Ya Taa (Sh/Lita)
Dar es Salaam	1,768	1,708	1,657
Arusha	1,852	1,791	1,741
Arumeru (Usa West)	1,852	1,791	1,741
Karatu	1,871	1,810	1,759
Monduli	1,858	1,797	1,746
Ngorongoro (Loliondo)	1,909	1,848	1,797
Kibaha	1,773	1,712	1,661
Bagamoyo	1,779	1,719	1,668
Kisarawe	1,776	1,715	1,664
Mkuranga	1,778	1,717	1,666
Rufiji	1,796	1,735	1,684
Dodoma	1,827	1,766	1,715
Bahi	1,834	1,774	1,723
Chemba	1,853	1,793	1,742
Kondoa	1,860	1,799	1,748
Kongwa	1,824	1,763	1,712
Mpwapwa	1,828	1,767	1,716
Iringa	1,832	1,771	1,721
Kilolo	1,837	1,776	1,725
Mufindi (Mafinga)	1,842	1,782	1,731
Njombe	1,860	1,800	1,749
Ludewa	1,898	1,838	1,787

Makete	1,891	1,831	1,780
Wanging'ombe (Igwachanya)	1,858	1,798	1,747
Bukoba	1,983	1,922	1,872
Biharamulo	1,958	1,897	1,846
Karagwe (Kayanga)	2,000	1,939	1,888
Kyerwa (Ruberwa)	2,005	1,945	1,894
Muleba	1,983	1,922	1,872
Ngara	1,949	1,888	1,837
Misenyi	1,992	1,931	1,880
Geita	1,933	1,873	1,822
Bukombe	1,922	1,862	1,811
Chato	1,954	1,894	1,843
Mbogwe	1,971	1,911	1,860
Nyang'hwale	1,948	1,888	1,837
Kigoma	1,999	1,938	1,887
Uvinza (Lugufu)	2,011	1,951	1,900
Buhigwe	1,988	1,928	1,877
Kakonko	1,956	1,896	1,845
Kasulu	1,985	1,924	1,873
Kibondo	1,964	1,903	1,852
Moshi	1,842	1,781	1,730
Hai (Bomang'ombe)	1,845	1,784	1,733
Mwanga	1,835	1,774	1,723
Rombo (Mkuu)	1,863	1,802	1,751
Same	1,828	1,767	1,717
Siha (Sanya Juu)	1,849	1,788	1,737
Lindi	1,827	1,766	1,715
Kilwa Masoko	1,802	1,741	1,690
Liwale	1,848	1,787	1,736
Nachingwea	1,856	1,795	1,744
Ruangwa	1,854	1,793	1,743
Babati	1,891	1,830	1,779
Hanang (Katesh)	1,901	1,840	1,789
Kiteto (Kibaya)	1,902	1,841	1,790
Mbulu	1,903	1,842	1,791
Simanjiro (Orkasumet)	1,922	1,862	1,811
Musoma	1,947	1,886	1,835
Rorya (Ingirijuu)	1,955	1,895	1,844
Bunda	1,938	1,877	1,826
Butiama	1,943	1,883	1,832

Serengeti (Mugumu)	1,992	1,931	1,880
Tarime	1,958	1,897	1,846
Mbeya	1,875	1,814	1,763
Chunya	1,885	1,824	1,773
Ileje	1,888	1,828	1,777
Kyela	1,891	1,830	1,779
Mbarali (Rujewa)	1,859	1,799	1,748
Mbozi (Vwawa)	1,885	1,824	1,773
Momba (Chitete)	1,893	1,833	1,782
Rungwe (Tukuyu)	1,884	1,823	1,772
Morogoro	1,793	1,732	1,682
Mikumi	1,809	1,748	1,697
Kilombero (Ifakara)	1,831	1,770	1,719
Ulanga (Mahenge)	1,842	1,781	1,730
Kilosa	1,812	1,751	1,700
Gairo	1,812	1,751	1,700
Mvomero (Wami Sokoine)	1,804	1,743	1,692
Turian	1,818	1,758	1,707
Mtwara	1,841	1,780	1,729
Nanyumbu (Mangaka)	1,889	1,829	1,778
Masasi	1,866	1,805	1,754
Newala	1,873	1,812	1,761
Tandahimba	1,866	1,805	1,754
Mwanza	1,918	1,857	1,806
Kwimba	1,954	1,893	1,842
Magu	1,926	1,865	1,814
Misungwi	1,924	1,863	1,812
Sengerema	1,951	1,890	1,839
Ukerewe	1,978	1,917	1,866
Sumbawanga	1,941	1,880	1,829
Kalambo (Matai)	1,933	1,873	1,822
Nkasi (Namanyele)	1,954	1,894	1,843
Katavi (Mpanda)	1,976	1,915	1,864
Mlele (Inyonga)	1,954	1,893	1,842
Songea	1,892	1,831	1,780
Mbinga	1,925	1,864	1,813
Namtumbo	1,921	1,860	1,809
Nyasa (Mbamba Bay)	1,927	1,867	1,816
Tunduru	1,950	1,889	1,839
Shinyanga	1,897	1,836	1,785
Kahama	1,911	1,850	1,799

Kishapu	1,925	1,865	1,814
Simiyu (Bariadi)	1,938	1,878	1,827
Busega (Nyashimo)	1,931	1,871	1,820
Itilima (Lagangabilili)	1,941	1,881	1,830
Maswa	1,930	1,869	1,818
Meatu (Mwanhuzi)	1,937	1,876	1,825
Singida	1,859	1,798	1,747
Iramba	1,871	1,810	1,759
Manyoni	1,843	1,783	1,732
Ikungi	1,854	1,794	1,743
Mkalama (Nduguti)	1,883	1,823	1,772
Tabora	1,922	1,861	1,810
Igunga	1,876	1,815	1,764
Kaliua	1,940	1,880	1,829
Ulyankulu	1,934	1,874	1,823
Nzega	1,887	1,826	1,775
Sikonge	1,934	1,873	1,822
Urambo	1,935	1,874	1,824
Tanga	1,814	1,754	1,703
Handeni	1,794	1,733	1,682
Kilindi	1,828	1,768	1,717
Korogwe	1,807	1,747	1,696
Lushoto	1,817	1,756	1,705
Mkinga (Maramba)	1,829	1,768	1,717
Muheza	1,814	1,754	1,703
Pangani	1,821	1,760	1,709

B: BEI ZA JUMLA

Bei za Jumla - DSM	Petroli (Sh/L)	Dizeli (Sh/L)	Mafuta ya Taa (Sh/L)
Bei Kikomo	1,666.43	1,605.52	1,554.59

Felix Ngamlagosi
MKURUGENZI MKUU
EWURA